

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

25/06/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA AZIDI KUUNGWA MKONO KAMPENI YA MATIBABU YA UPASUAJI MOYO KWA WATOTO, ACHANGIWA MILIONI 13 NA WASAMARIA WEMA.

Kampeni ya Matibabu ya upasuaji wa moyo kwa watoto 60 kutoka familia zenye maisha duni iliyoanzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda imezidi kugusa Mioyo ya wadau na watu mbalimbali ambapo leo Kampuni ya Ako Group Ltd imeahidi kutoa mchango Shilingi Milioni10 kwa ajili ya matibabu ya watoto watano huku wanachama wa Chama cha Washehereshaji Tanzania wakichangia kiasi Cha Shilingi milioni 3.3 kwa ajili ya matibabu kwa watoto wenye tatizo la moyo.

RC Makonda amesema fedha hizo zitawezesha matibabu ya upasuaji wa moyo kwa Watoto saba ambapo ametoa wito kwa wadau, taasisi na kampuni mbalimbali kusaidia matibabu ili kuokoa maisha yao.

Hayo yamejiri wakati wa mkutano mkuu wa Chama cha Washehereshaji ambapo katika michango hiyo kampuni ya Ako Group Ltd imetoa ahadi ya kusaidia matibabu ya watoto watano na chama cha washehereshaji kimejitolea kugharamia matibabu kwa watoto wawili na kufanya idadi kuwa watoto saba .

Itakumbukwa Jumamosi ya Juni 22 RC Makonda alitoa ufadhili wa matibabu ya upasuaji wa moyo kwa watoto kumi kati ya sitini ikiwa ni mkakati wake wa matibabu ya watoto kumi kila mwezi.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM